AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

Arusha, Tanzania

Tovuti: www.african-court.org

Simu: +255-272-510-510

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**ABDUL OMARY NONDO NA WENGINE**

**DHIDI YA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI Na. 040/2020 & 043/2020**

**(MAOMBI YALIYOUNGANISHWA)**

**HUKUMU KUHUSU UZINGATIAJI WA SHERIA NA FIDIA**

**6 MACHI 2026**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, 6 Machi 2026**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) leo imetoa hukumu katika kesi ya *Abdul Omary Nondo na Wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

Abdul Omary Nondo, Deusdedit Valentine Rweyemamu na Paul Revocatus Kaunda (hapa wanarejelewa kama "Mleta Maombi wa Kwanza," "Mleta Maombi wa Pili," na "Mleta Maombi wa Tatu" mtawalia au "Waleta Maombi" kwa pamoja) wote ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ("Mjibu Maombi"). Waliwasilisha Maombi yao dhidi ya Mjibu Maombi wakipinga vifungu mbalimbali katika sheria za uchaguzi za Tanzania. Mahakama, ikitenda *kwa hiari yake*, iliamuru Maombi hayo mawili yaunganishwe baada ya kubaini kufanana kwa malalamiko ya Waleta Maombi na suluhu zinazotafutwa.

Mjibu Maombi alipinga mamlaka ya Mahakama pamoja na ukubalifu wa Maombi haya.

Kuhusiana na mamlaka ya Mahakama, Mjibu Maombi alipinga mamlaka ya muda ya Mahakama. Kwa umahususi, Mjibu Maombi alisema kwamba Maombi hayo yalitokana na vifungu vya kikatiba vilivyopitishwa mwaka 1977 na 1984, kabla ya kuanza kutumika kwa Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu ya Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ("Itifaki"). Aidha, Mjibu Maombi alidai kwamba, wakati huo, alikuwa hajaweka Azimio chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki.

Kuhusu madai kwamba ukiukwaji unaodaiwa kufanywa ulitokea kabla ya kuanza kutumika kwa Itifaki na kuweka Azimio, Mahakama ilisisitiza msimamo wake kwamba mamlaka yake ya muda huamuliwa kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Itifaki iliyoianzisha, na si kuanzia tarehe ya kuweka Azimio, uwekaji Azimio unahusiana tu na mamlaka yake binafsi. Mahakama pia ilibainisha kuwa kama kighairi cha kanuni hii, ina mamlaka ya kisheria katika matukio ambapo ukiukaji ulitokea kabla ya Nchi kuwa mhusika wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu ("Mkataba") au Itifaki, lakini ukiukaji unaodaiwa kufanywa umeendelea hadi baada ya Mkataba na Itifaki kuanza kutumika.

Katika hali hiyo, Mahakama ilibaini kuwa ukiukaji unaodaiwa na Waleta Maombi ulikuwa endelevu na hivyo kuipa mamlaka ya muda ya kusikiliza na kuamua Maombi haya.

Ingawa vipengele vingine vya mamlaka yake havikupingwa na Mjibu Maombi, hata hivyo, Mahakama iliviangalia kwa mujibu wa Kanuni ya 49(1) ya Kanuni za Mahakama ("Kanuni").

Kuhusiana na mamlaka binafsi, Mahakama ilibainisha kuwa Mjibu Maombi aliweka Azimio chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki, ambacho kinaruhusu watu binafsi kuwasilisha Maombi dhidi yake, kulingana na Kifungu cha 5(3) cha Itifaki. Mahakama ilirejelea zaidi kwamba Mjibu Maombi aliondoa Azimio lake mnamo tarehe 21 Novemba 2019. Kuhusiana na hili, Mahakama ilisisitiza kwamba kuondolewa kwa Azimio hakukuathiri Maombi ya sasa kwani uondoaji huo ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 22 Novemba 2020, ambapo Maombi haya yalikuwa yamewasilishwa tayari.

Mahakama ilibainisha pia kwamba kulingana na kwamba ukiukaji unaodaiwa kufanywa unahusu haki zilizowekwa katika Mkataba na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR), hati ambazo Mjibu Maombi ameridhia, ilikuwa na mamlaka muhimu ya kuchunguza Maombi haya.

Mwisho, Mahakama ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya kieneo, ikizingatiwa kuwa ukweli wa jambo hilo ulitokea ndani ya eneo la Mjibu Maombi.

Kuhusu ukubalifu wa Maombi, Mahakama iliona kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Itifaki, lazima iamue kuhusu ukubalifu wa Maombi yote yaliyowasilishwa mbele yake. Mjibu Maombi aliibua pingamizi kwa madai kwamba Waleta Maombi walishindwa kuwasilisha Maombi haya ndani ya muda mwafaka kwa mujibu wa Kifungu cha 56(6) cha Mkataba.

Kuhusiana na pingamizi hili, Mahakama iliona kwamba chini ya Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama, kuna vipengele viwili ambavyo lazima vitumike katika kutathmini uhalali wa muda wa kuwasilisha Maombi. Kwanza, Maombi lazima yawasilishwe ndani ya muda mwafaka kuanzia tarehe ambayo taratibu za ndani zilikamilia. Pili, na kama njia mbadala, Maombi lazima yawasilishwe ndani ya muda mwafaka kuanzia tarehe iliyowekwa na Mahakama kuwa mwanzo wa muda ambao shauri hilo litafikishwa katika Mahakama.

Katika maombi haya, Mahakama iliona kwamba Waleta Maombi hawakulazimika kukamilisha taratibu za ndani si tu kwa sababu hakukuwa na taratibu hizo za kukamilisha bali pia kwa sababu baadhi ya ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulikuwa endelevu. Kwa hivyo, hesabu ya muda haikuwekwe katika utimilifu wa taratibu za ndani kwani utimilifu huo haukuwa muhimu. Kuhusu kipengele cha pili, Mahakama iliona kwamba kutokana na iliyoyabaini kuhusu ukiukaji unaoendelea, Waleta Maombi wangeweza kuwasilisha Maombi haya wakati wowote ilimradi ukiukaji huo uliendelea kuwepo. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Maombi haya yalitimiza matakwa ya ukubalifu, na ilitupilia mbali pingamizi la Mjibu Maombi.

Mahakama iliona kwamba hakuna pingamizi lililotolewa kuhusiana na matakwa mengine ya ukubalifu. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Mahakama, Mahakama ilitathmini vigezo vyote vya ukubalifu vilivyoainishwa katika Kanuni ya 50(2) ya Kanuni za Mahakama ili kuhakikisha kwamba Maombi haya yanakidhi matakwa muhimu.

Kwa hivyo, Mahakama ilibaini kuwa sharti lililowekwa chini ya Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni za Mahakama lilitimizwa, kwa kuwa Waleta Maombi walitambuliwa kwa udhahiri kwa majina yao.

Mahakama ilibaini pia kwamba lugha iliyotumika katika Maombi husika haikuwa ya dharau au ya matusi kwa Mjibu Maombi au taasisi zake katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni za

Mahakama. Maombi haya pia hayakutoka tu na habari zinazosambazwa kupitia vyombo vya habari kwani yalitokana na nyaraka za mahakama kutoka mahakama za ndani za Mjibu Maombi katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni za Mahakama.

Aidha, Mahakama ilibainisha kwamba madai ya Waleta Maombi yalilenga kulinda haki zao zilizohakikishwa kwa mujibu wa Mkataba. Pia ilibainisha kuwa katika Maombi haya, hakukuwa na jambo ambalo lilikuwa kinyume cha Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Maombi haya yalikidhi matakwa ya Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni za Mahakama.

Mahakama pia ilibaini kuwa kesi hiyo haikuwa imeshughulikiwa hapo awali baina ya wahusika mbele ya mahakama nyingine ya kimataifa na kwa hivyo ilikidhi Kanuni ya 50(2)(g) ya Kanuni za Mahakama.

Kuhusiana na kukamilisha taratibu za ndani, Mahakama ilirejelea kwamba lengo la kanuni kuhusu kukamilisha taratibu za ndani chini ya Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama ni kuzipa Nchi fursa ya kushughulikia kesi za madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu ndani ya mamlaka zao kabla shirika la kimataifa la haki za binadamu kuombwa kuamua kuhusu jukumu Serikali, kwa mujibu wa kanuni ya kukamilisha kwanza taratibu za ndani. Mahakama pia ilirejelea kwamba sharti la kukamilisha taratibu za ndani linahusu kwamba Mleta Maombi lazima angalau awe amewasilisha madai hayo mbele ya Mahakama katika mahakama za ndani. Katika Maombi haya, Mahakama ilibainisha kwamba Waleta Maombi walitoa madai matano dhidi ya sheria za uchaguzi za Mjibu Maombi. Mahakama ilitathmini kila moja ya madai hayo ili kuamua endapo taratibu za ndani zilikamilika.

Kwanza, Mahakama iliangalia madai yanayohusiana na muundo wa Tume ya Uchaguzi, ambao Waleta Maombi walidai ulikiuka kifungu cha 74(1) cha Katiba ya Mjibu Maombi, Kifungu cha 1, 3, 13(1) cha Mkataba, Kifungu cha 21 cha Tamko la Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu (UDHR) na Kifungu cha 25 cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR). Waleta Maombi waliwasilisha kwamba wasingeweza kufika Mahakama Kuu kwa mujibu wa Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu, ikizingatiwa kuwa vifungu vya

kikatiba wanavyovipinga viko nje ya Sura ya III ya Sehemu ya Kwanza ya Katiba ya Mjibu Maombi.

Mahakama ilibainisha kuwa madai ya Waleta Maombi yanayohusu muundo wa Tume ya Uchaguzi, kufikia wakati wa kuwasilisha Maombi, yaliongozwa na Katiba ya Mjibu Maombi na Sheria ya Uchaguzi wa Kitaifa. Mahakama ilibaini kwamba Waleta Maombi hawakuwahi kufika kwenye mahakama yoyote ya ndani kwa ajili ya kuamua malalamiko yao, na hivyo iliona kwamba Waleta Maombi walishindwa kukamilisha taratibu za ndani kuhusiana na madai yao yanayohusiana na Kifungu cha 74(1) cha Katiba ya Mjibu Maombi. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba dai hilo haliwezi kusikilizwa kwa sababu ya kushindwa kukamilisha taratibu za ndani.

Pili, Mahakama iliangalia suala la kukamilisha taratibu za ndani kuhusiana na madai kwamba jinsi kifungu cha 74(3) cha Katiba ya Mjibu Maombi kinavyobainisha wale wanaostahili kutumika katika Tume ya Uchaguzi kinakiuka haki za Waleta Maombi chini ya Kifungu cha 1, 3, 13(1) cha Mkataba, Kifungu cha 21 cha UDHR na Kifungu cha 25 cha ICCPR.

Kuhusu madai haya, Mahakama iliona kwamba Waleta Maombi walishindwa kuonyesha kwamba walijaribu kukamilisha taratibu za ndani kwa hivyo iliona kwamba madai hayo hayawezi kusikilizwa kwa sababu ya kushindwa kukamilisha taratibu za ndani.

Tatu, Mahakama iliangalia endapo Waleta Maombi walikamilisha taratibu za ndani kuhusiana na kuondolewa kwa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi. Kuhusu madai haya, Waleta Maombi walidai kwamba kifungu cha 74(5) cha Katiba ya Mjibu Maombi kinaathiri uhuru wa Tume ya Uchaguzi kwa kumpa Rais mamlaka ya kumwondoa madarakani mjumbe wa Tume ya Uchaguzi kulingana na atakavyoona na kwa sababu zisizo dhahiri.

Kuhusu suala hili, Mahakama pia ilibaini kwamba Waleta Maombi hawakutoa ushahidi wowote kuonyesha kwamba walikamilisha taratibu za ndani, kwa hivyo iliona kwamba Maombi haya hayakukidhi matakwa ya kukamilisha taratibu za ndani kuhusiana na madai haya.

Nne, Mahakama iliangalia endapo Maombi yalikidhi matakwa ya kukamilisha taratibu za ndani kuhusiana na madai yanayohusiana na mamlaka ya mahakama ya kuhoji hatua zinazochukuliwa na Tume ya Uchaguzi. Waleta Maombi walidai kuwa kifungu cha 74(12) cha katiba ya Mjibu Maombi na kifungu cha 119(13) cha Katiba ya Zanzibar vinakiuka kanuni za usawa mbele ya sheria na ulinzi sawa wa sheria kama ilivyoelezwa chini ya Kifungu cha 3 cha Mkataba na kifungu cha 14(1) cha ICCPR. Waleta Maombi pia walidai kwamba vifungu hivyo vinakiuka Kifungu cha 7(1)(a) cha Mkataba na Kifungu cha 14(1) cha ICCPR kwa kuondoa mamlaka ya mahakama katika nchi ya Mjibu Shauri.

Kuhusiana na madai haya, Mahakama ilirejelea maamuzi yake ya awali, ikibaini kwamba vifungu vinavyoondoa mamlaka ya mahakama vinawanyima walalamikaji njia za kuleta suluhu. Mahakama ilibaini kwamba kutokana na masharti ya Kifungu cha 74(12) cha Katiba ya Mjibu Maombi na Kifungu cha 119(13) cha Katiba ya Zanzibar, Waleta Maombi hawakuwa na njia ya suluhu iliyokuwepo, inayojitosheleza na yenye ufanisi kuweza kuikamilisha kabla ya kufika kwenye Mahakama hii. Kwa hivyo Mahakama iliona kwamba Maombi haya yalikidhi matakwa ya ukubalifu kuhusiana na madai haya.

Tano, Mahakama iliangalia endapo Maombi haya yalikidhi matakwa ya ukubalifu kuhusiana na madai kwamba marufuku ya kujiunga na vyama vya siasa kwa watu wanaohusika katika usimamizi wa uchaguzi ilikiuka Kifungu cha 1, 3, 13(1) cha Mkataba, Kifungu cha 21 cha UDHR na Kifungu cha 25 cha ICCPR.

Kuhusiana na madai haya, Mahakama ilibainisha kwamba Waleta Maombi walikuwa wameshindwa kutoa ushahidi wowote kuhusu kukamilisha taratibu za ndani, au kuonyesha kwamba taratibu hizo hazikupatikana. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Waleta Maombi hawakukamilisha taratibu za ndani kuhusu madai yanayohusiana na kifungu cha 74(14) cha Katiba ya Mjibu Maombi, na iliona kwamba Maombi haya hayakukidhi matakwa yanayohusu kukamilisha taratibu za ndani.

Baada ya kutathmini matakwa yote yanayohusiana na kukamilisha taratibu za ndani, Mahakama iliona kwamba Maombi haya yalitimiza matakwa hayo kwenye madai

yanayohusiana na kifungu cha 74(12) cha Katiba ya Mjibu Maombi na kifungu cha 119(13) cha Katiba ya Zanzibar.

Kisha Mahakama iliangalia endapo kifungu cha 74(12) cha Katiba ya Mjibu Maombi na kifungu cha 119(13) cha Katiba ya Zanzibar vilikiuka kanuni za usawa mbele ya sheria na ulinzi sawa wa sheria kama inavyolindwa chini ya Kifungu cha 3 cha Mkataba na Kifungu cha 14(1) cha ICCPR. Mahakama pia iliangalia madai ya Waleta Maombi kwamba vifungu hivyo vya kikatiba vinakiuka haki ya mtu kusikilizwa kama inavyolindwa chini ya kifungu cha 7 cha Mkataba.

Kuhusu madai ya ukiukaji wa haki ya usawa na ulinzi sawa wa sheria, Mahakama ilisisitiza kwamba kanuni ya usawa mbele ya sheria inataka kwamba sheria imlinde kila mtu bila ubaguzi. Mahakama ilirejelea pia kwamba, kuhusiana na masharti ya Kifungu cha 74(12) cha Katiba ya Mjibu Maombi na Kifungu cha 119(13) cha Katiba ya Zanzibar, katika kesi ya *Jebra Kambole dhidi ya Tanzania*, iliamua kuhusu kifungu kama hicho katika Katiba ya Mjibu Maombi, ambacho kiliondoa mamlaka ya mahakama kusikiliza malalamiko yoyote yanayohusiana na uchaguzi wa Rais katika nchi ya Mjibu Maombi. Sheria hiyo ilichukuliwa kuwa ni ukiukaji wa Mkataba bila uhalali wa kutosha katika jamii ya kidemokrasia. Kutumia hoja kama hiyo Mahakama ilibaini kuwa vifungu vya katiba vinavyopingwa vinaondoa mamlaka ya mahakama kuhoji hatua zinazochukuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Mjibu Maombi (NEC) na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC). Mahakama ilibaini kuwa ingawa vifungu vinavyopingwa kimsingi vinawahusu raia wote katika nchi ya Mjibu Maombi, matokeo yake halisi hayafanani kwa watu wote. Kwa mujibu wa Mahakama, sheria hizo zina athari kubwa kwa watu wanaotafuta suluhu ya kisheria kwa malalamiko yanayohusiana na uchaguzi yanayoweza kutokea kutokana na watu hao kutokuwa na uwezo wa kupinga matokeo ya uchaguzi mbele ya chombo cha mahakama. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba kifungu cha 74(12) cha katiba ya Mjibu Maombi na kifungu cha 119(13) cha Katiba ya Zanzibar vinakiuka Kifungu cha 3(2) cha Mkataba.

Kuhusu madai ya ukiukaji wa haki ya mtu kusikilizwa, Mahakama ilirejelea uamuzi wake wa awali katika kesi ya *Jebra Kambole dhidi ya Tanzania*, ambapo iliona vizuizi vilivyo katika kifungu cha 41(7) cha Katiba ya Mjibu Maombi kuwa vinapingana na Kifungu cha 7(1)(a) cha Mkataba. Mahakama, katika kesi ya *Jebra Kambole dhidi ya Tanzania*, ilisisitiza kwamba

wakati wowote ambapo Serikali inaweka kizuizi kwenye haki za msingi, inabeba mzigo wa kuthibitisha kwamba kizuizi hicho kimewekwa kisheria kwa mujibu wa sheria, kinatimiza kusudi halali, na ni cha lazima na faafu kutimiza kusudi hilo. Aidha, Mahakama imesisitiza kwamba Nchi haiwezi kutaja sheria zake za ndani kuhalalisha kutofuata wajibu wake wa kimataifa wa haki za binadamu. Kutokana na hayo, Mahakama ilibaini kuwa NEC na ZEC kutohojiwa mahakamani kunaleta hatari ya kasoro za uchaguzi kutoshughulikiwa, na hivyo kudhoofisha utawala wa sheria. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba kifungu cha 74(12) cha katiba ya Mjibu Maombi na kifungu cha 119(13) cha Katiba ya Zanzibar, kwa kadiri ambavyo vinaiondoa mahakama kuhoji matokeo ya NEC na ZEC vinakiuka Kifungu cha 7(1)(a) cha Mkataba.

Kuhusu madai ya ukiukaji wa Kifungu cha 1 cha Mkataba, Mahakama ilirejelea kwamba inapoona kwamba haki, wajibu na uhuru wowote kwa mujibu wa Mkataba umepunguzwa, umekiukwa au haujatimizwa, inamaanisha kwamba wajibu uliowekwa kwa mujibu wa Kifungu cha 1 cha Mkataba umekiukwa. Kwa hivyo Mahakama iliona kwamba Mjibu Maombi alikiuka Kifungu cha 3(2), 7(1)(a) na 1 cha Mkataba.

Baada ya kuona kwamba sehemu za kifungu cha 74(12) na kifungu cha 119(13) zinakiuka Kifungu cha 3 (2) na 7 (1) (a) cha Mkataba, Mahakama iliamuru Mjibu Maombi achukue hatua zote muhimu za kikatiba na kisheria, ndani ya muda unaofaa, na katika hali yoyote ndani ya miezi 24 baada ya kupewa taarifa ya uamuzi, kuhakikisha kwamba sheria hizi zinarekebishwa na zinazingatia masharti ya Mkataba ili kuondoa ukiukaji wa Kifungu cha 3(2) na 7(1)(a) cha Mkataba kama ilivyoamuliwa na Mahakama.

Aidha, Mahakama iliamuru kwamba Mjibu Maombi achapishe hukumu hii kwa Kiswahili na Kiingereza, ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu tarehe ya kupokea taarifa, kwenye tovuti za Mahakama, na Wizara ya Katiba na Sheria, na kuhakikisha kuwa hati ya hukumu inapatikana kwa angalau mwaka mmoja baada ya tarehe ya kuchapishwa.

Kuhusu utekelezaji na kutoa ripoti, Mahakama iliamuru Mjibu Maombi awasilishe kwake ripoti kuhusu hali ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa ndani ya miezi sita tangu tarehe ya taarifa

ya hukumu hii kutolewa, na baada ya hapo, kila baada ya miezi sita hadi Mahakama itakapoona kuwa kumekuwa na utekelezaji kamili.

Kuhusu gharama, Mahakama iliamuru kwamba kila mhusika abebe gharama zake.

Maelezo zaidi

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, yanaweza kupatikana kwenye tovuti kupitia: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0402020

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.